CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCE AND TECHNOLOGY

A constituents of Chato health foundation Tanzania Limited

P.O. Box 73, Chato – Geita – Tanzania
Tel: +255 767 638495 / +255 784 616788/ +255769741336
Website:www.chatocollege.ac.tz: email: chatocohest@gmail.com

Kumb. Na: **HAS.158/05/017**
Tarehe: ..... /...../2017

Kwa Ndugu:

.....**.....**

.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA / ASTASHAHADA YA UTABIBU KWA MWAKA 2017/2018
(TECHNICIAN CERTIFICATE IN CLINICAL MEDICINE)

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na
mafunzo ya Stashahda/Astashahada ya utabibu kwa muda wa miaka miwili/mitatu katika chuo cha sayansi ya Afya na Technolojia Chato kilichopo Mkoa wa Geita katika Wilaya ya Chato kwa mwaka wa masomo 2017/2018.
Kwa barua hii unatakiwa kuripoti chuoni siku ya Jumatano **tarehe 20/09/2017** kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:30 jioni kwa ajili ya usajili na Masomo yataanza **ndani ya Siku saba tangu tarehe ya kuripoti.**

Ikumbukwe kuwa kama hautafika katika muda uliotajwa hautapokelewa na nafasi yako itajazwa na mtu mwingine. Chuo kina Hosteli za wanaume na wanawake, Uamuzi wa kukaa Hosteli (Boarding) au
kusoma ukitokea nyumbani (Day) ni hiari yako.

1. <u>MALIPO</u>

- Ada za kozi kwa mwaka ni **Tsh. 2,300,000/=** nje ya Gharama za Hosteli.
- Kwa atakayehitaji kukaa Hosteli ni Tshs . 300,000/= kwa mwaka Ikiwa ni nje ya Gharama ya Chakula.

- Chuo kina utaratibu mzuri wa Chakula hapohapo chuoni kwa gharama ya Tshs.**380,000/=** kwa muhula na inalipwa kwa kila mwanzo wa muhula unapoanza ili kufanya maandalizi ya chakula.
- Kama mwanafunzi hana kadi ya mfuko wa taifa wa Bima ya Afya ni lazima alipie kiasi cha Tshs. **54,000/**= mara tu afikapo chuoni ili fomu yake ipelekwe kwa maandalizi ya kupata kadi ya matibabu na inalipwa kwa kila mwaka unapoanza.

Malipo ya Ada pamoja na Hostel yalipwe Benki ya **NMB** tawi la Chato kwenye akaunti ya Chuo Namba**. 32710008227,** Jina la akaunti ni **CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCE AND TECHNOLOGY**

NB. Tafadhali malipo ya chakula yalipwe chuoni moja kwa moja.

Unasisitizwa kuripoti mapema ili taarifa zako zitumwe NACTE. Hakikisha unakuja na picha (4) za rangi (passport size) zilizopigwa hivi karibuni (Current passport size).

Mbali na Ada ya Chuo, *kila mwanafunzi atatakiwa kulipa sh.* ***280,000/=*** *kila mwaka kwenye akaunti ya wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika Benki ya* ***NMB Bank House BRANCH*** *akaunti namba* ***20110007946*** *yenye jina la* ***Application and Examination Fees kwa ajili ya gharama za mitihani ya kitaifa.fedha hizi zikishalipwa hazirudishwi kwa sababu yoyote ile, kumbuka kutochanganya akaunti ya Chuo na hii ya wizara ya Afya.***

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

i) Hatupokei fedha taslimu chuoni, malipo yote ya Ada yafanyike kupitia Benki tu.
ii) Hairuhusiwi kupika hostel wala kuonekana na jiko au vyombo vya kupikia sehemu hiyo.
iii) Hautapokelewa chuoni kama utakuja bila kukamilisha malipo na mahitaji yanayotakiwa.

3. MAHITAJI

Wanachuo wote wanatakiwa kuja na vitu vifuatavyo:-

- Cheti halisi pamoja na nakala cha kuhitimu kidato cha nne (Usilete vivuli peke yake).
- Vifaa vya kutosha vya kujifunzia kama vile Daftari (counter books) kalamu, rula n.k
- Vitabu vya rejea vinavyohusu kozi husika kama vile anatomy and physiology (ROSE & WILSON) na Medical Dictionary pindi unapokuwa mbali na maktaba ya chuo kwa ajili ya rejea n.k.

- Mwamvuli au koti kwa ajili ya matumizi wakati wa majira ya mvua au baridi.
- Nguo na viatu vya michezo.
- Taarifa ya kupima Afya (medical examination) kutoka kwenye hospital au kituo cha Afya Kinachotambulika (Fomu imeambatanishwa).
- Vitendea kazi wakati wa mafunzo kwa vitendo – clinical thermometer,stethoscope, Glucometer, BP machine (Manual), jozi moja ya viatu na mavazi maalum ya kuvaa chumba cha upasuaji
- Pattela hammer na clinical torch.
- Rimu mbili za karatsi A4 unapofika chuoni kwa ajiri ya mitihani ya kila mwezi na ile ya wiki.

KWA WANAFUNZI WA HOSTELI TU.

Yafuatayo ni mahitaji ambayo wanachuo watakaokaa Hosteli wanatakiwa kuja nayo:-

- Shuka 4, Blanketi 1, chandarua cha pembe nne kinachoenea kwenye kitanda cha ft 3, foronya 2 na taulo 1.
- Ndoo moja ya plastic ya lita 20, beseni la plastic lenye ukubwa wa kati na Sanduku au Begi la kutunzia vitu vya thamani lenye kufungwa na kufuli kwa ajili ya usalama binafsi.
- Fedha kwa ajili ya malipo ya Hostel Tshs. 300,000/= (laki tatu tu)
- Fedha ya chakula inalipwa kantini kwa kila mwezi Tshs.105,000/= (Laki moja na elfu tano) au unaweza kulipa kwa muhula Tshs 380,000/= ili upate unafuu wa miezi sita.

4. SARE:

Wanachuo wote wa kutwa na wa Hosteli watatakiwa kuja na sare zilizoshonwa vizuri za vitambaa vya aina ya pamba au tetron nzito zisizokuwa na mistari, maua wala vidotidoti zinazokidhi maadili ya taaluma ya uganga na pia kwa jamii pia nguo zinazoonyesha maumbile hazitaruhusiwa.

WANAUME:-

- Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- Suruali mbili za rangi ya khaki.
- Makoti mawili meupe (clinical coats) ya mikono mirefu kwa ajiri ya kazi za wodini/Hospitalini.
- Viatu vyeusi aina ya ngozi.

WANAWAKE:-

- Magauni mawili meupe yenye mikono mifupi.

- ❖ Makoti mawili meupe(clinical coats) ya mikono mirefu kwa ajiri ya kazi za wodini/Hospitalini.
- ❖ Viatu vyeupe au vyeusi aina ya ngozi.

5. HUDUMA YA CHAKULA

Chakula kinapatikana kwa malipo ya Tsh 380,000/= kwa kila muhula (chai,chakula cha mchana na Usiku).

6. MATIBABU

Chuo kinatumia mfumo wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) kwa kupata matibabu katika Hospitali yetu ya wilaya ambayo ndiyo Hospitali ya mafunzo kwa wanachuo wote.

7. ULINZI NA USALAMA

Ili kuhakikisha usalama wa mali na vitu vya Wanachuo na Watumishi , chuo kina ulinzi wa kutosha katika mazingira ya Chuo,hata hivyo wilaya ya Chato ina usalama wa kutosha kwa mazingira yote.

8. SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

Chuo kina sheria na taratibu mbalimbali zilizowekwa kwa ajili ya kudumisha nidhamu za wanachuo wakati wa mafunzo ili kusaidia kuleta maadili yaliyokusudiwa katika taaluma inayofundishwa. Chuo kinatumia sheria za Wizara ya Afya kwa ajili ya vyuo vyote vya Afya Tanzania Bara.

Kwa hiyo wanachuo wote watatakiwa kuzisoma vizuri sheria hizo mara tu wafikapo chuoni na kuzizingatia siku zote. Baada ya kusomewa /kuzisoma sheria hizo kila mwanafunzi atatakiwa kusaini kopi yake na itatunzwa kwenye faili la kila mwanafunzi.

9. JINSI YA KUFIKA CHUONI

Chuo kipo eneo la Mbuye katika kata ya Bwina chato mjini wilaya ya Chato Mkoa wa Geita.

“Uwapo nasi Afya imezingatiwa”.

.....

Dr Stanslaus Kiyicha.

MKUU WA CHUO

Chato College of Health Science and Technology

ATTACHMENT – A

A: TUITION FEES (ADA YA MAFUNZO):- TSHS **2,300,000**/= Kwa Mwaka unaweza kuilipa kwa awamu mbili yaani **1,150,000**/= kwa muhula mmoja.

B: OTHER CHARGES:

These are the other charges which must be paid on the same day of reporting which is direct payment toreception or separate pay in Slip and no installment is allowed to this amount (one-time payment).

Except NHIF if already NHIF beneficiary, who will show the treatment Card during registration.

EXPLANATION	**AMOUNT (Tshs.)**
Identity Card Fees	10,000.00
T-Shirt	20,000.00
Books fee	50,000.00
Student's Union fees	10,000.00
Treatment Fees -NHIF (Optional)	54,000.00
NACTE Quality Assurance fee	15,000.00
TOTAL	**159,000.00**

TOTAL COSTS FROM COLUM A & B ABOVE = 2,459,000/= Excluding Accommodation expenses and Ministry of Health examination fees (280,000/=

CODE OF CONDUCT:

Chato college of Health Science and Technology believes in equal opportunity and does not discriminate against any student or prospective student on the basis of race, sex, origin disability or religion. Thus, you are supposed to abide with the college rules and regulations attached to this letter and sign below if you agree and accept the offer.

You are warmly welcome and I wish you God's blessings through your academic work at the centre.

KIAMBATANISHO -B

KANUNI NA SHERIA ZA CHUO CHA SAYANSI YA AFYA NA TEKNOLOJIA CHATO

1. Kwa miaka yote ya masomo mwanafunzi haruhusiwi kuwa na shughuli nyingine zissizohusiana na masomo yaliyomleta hapa Chuoni.
2. Ni lazima mwanafunzi afuate sheria, maadili na taratibu za jamii wakati wote wa masomo yake hapa Chuoni.
3. Kazi zisizo za lazima kama kufua, kupiga pasi n.k zifanyike Jumapili au Jumamosi isipokuwa kazi ya kutunza usafi wa mazingira.
4. Inawapasa wanafunzi wawe waaminifu daima; adhabu kali itatolewa kwa udanganyifu utakaofanyika wakati wowote..
5. Siku ya Soko mwanafunzi anaweza kuomba ruhusa kwa Dean kwenda kutafuta mahitaji maalum sokoni,na nilazima avae sare ya Chuo au T-shirt yenye nembo ya chuo.
6. Mgeni yeyote wa mwanafunzi haruhusiwi kuingia bwenini/Hospital , akae sehemu maalum ya wageni. Baada ya saa 12:00 jioni mgeni haruhusiwi kuwepo kwenye maeneo la Chuo/Hospital na siku za wageni ni Jumamosi na Jumapili tu kuanzia saa 07:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.kwa wanafunzi wanokaa bwenini.
7. Mwanafunzi atawajibika kufanya usafi {IPC} wa bweni lake, darasa, viwanja vya Chuo/Hospital na sehemu zingine atakazopangiwa na uongozi wa Chuo/Hospitali.
8. Radio na vyombo vya muziki haviruhusiwi chuoni.
9. Kwa wale wanaotoka mbali Chuo kitatoa sehemu ya malazi bweni kwa Tsh [300,000/] laki tatu tu kwa Mwaka na chakula kitatolewa kwa kulipia Tshs 105.000/= (laki Moja na elfu tano tu kwa mwezi mmoja) na mwanafunzi anaweza kujitegemea pia chakula akiwa hosptel.
10. Kila mwanafunzi atapewa likizo ya siku ishirini na nane (28) au wiki nne (4) kwa mwaka na siku kumi na nne (14) au wiki mbili kabla ya kuanza mwaka mpya wa masomo. Siku ishirini (20) za ugonjwa ndani ya miaka mwili (2) zinakubalika. Siku kumi na nne (14) zaidi ya hapo hatafanya mtihani wa kuhitimu wa Serikali.
11. Mwanafunzi akikosekana majuma matatu (3) mfululizo Chuoni atarudia mwaka.
12. Mwanafunzi akiugua aende kwanza kwa Mwalimu wa Zamu/Warden ili apewe sick-sheet kabla ya kwenda kwa Mganga. Matibabu ya mwanafunzi ya ziada yatalipwa na yeye mwenyewe kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

13. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi wa kike au kiume kuwa na uhusiano wa kimapenzi/uchumba wakati wa masomo, ama sivyo wataachishwa masomo.
14. Mwanafunzi yeyote wa kike atakayepata mimba akiwa masomoni ataachishwa masomo kwa mwaka mmoja, na mwanafunzi wa kiume akijulikana amempatia mwanafunzi mwenzie wa kike mimba pia naye ataachishwa kwa muda wa mwaka mmoja.
15. Kila mwanafunzi lazima shiriki kikamilifu katika shughuli za kujitegemea (self-reliance). Mwanafunzi atakayeonyesha ulegevu, utoro na uzembe katika shughuli hizo atachukuliwa hatua kali.
16. Kila mwanafunzi analazimika kushiriki katika michezo (k.m. mpira) na shughuli za starehe (k.m kwaya, sanaa) kwani ni sehemu ya masomo.
17. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda na simu darasani au kazini.
18. Makosa yanayoweza kumwondoa mwanafunzi Chuoni ni kama yafuatayo:

    - Uasherati, Ulevi, Utoaji mimba, uvutaji sigara, kutumia bangi au dawa za kulevya
    - Matusi, ugomvi na kupigana
    - Kutowatii Walimu na Wakuu wa Hospitali
    - Wizi wa aina yoyote
    - Udanganyifu na uongo wa aina yoyote
    - Kutohudhuria darasani bila sababu maalum
    - Kuvunja taratibu, kanuni na sheria za nchi
19. Baada ya kusoma kanuni na sheria za Chuo, hakikisha umeweka saini katika sehemu yako hapa chini na mzazi/mlezi wako.

KIAMBATANISHO –C

NAKUBALIANA NA KANUNI/SHERIA ZILIZO KWENYE BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO HIKI NA NINA AHIDI KUYATEKELEZA VEMA.

Jina kamili la Mwanafunzi _____

Saini ya mwanafunzi _____

Jina la Mzazi/Mlezi _____

Saini ya Mzazi/Mlezi _____

Anuani ya Mzazi/Mlezi: _____

_____

_____

Simu: _____

Email: _____

KARIBU SANA KATIKA CHUO CHA SAYANSI YA AFYA NA TECHNOLOJIA CHATO ILI UPATE ELIMU BORA NA MAFANIKIO

CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCE AND TECHNOLOGY

Our Motto is: - COMMITMENT TO SUCCESS